JAMHURI YA MUUNGO WA TANZANIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A

612 **URAIA**

Muda: Saa 3 Hours **Mwaka: 2024**

Maelekezo

1. Karatasi hii ina Sehemu **A** na **B** zenye jumla ya maswali **kumi na manne (14).**
2. Jibu maswali **yote** kutoka Sehemu **A** na maswali **manne (4)** kutoka Sehemu **B**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na Sehemu **B** ina alama sitini **(60).**
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Toa hoja nne za umuhimu wa kuwa na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
2. Eleza sababu nne za kupigwa vita kwa mila ya ukeketaji.
3. Thibitisha kwa kueleza tabia nne za mtoto aliyekosa malezi stahiki.
4. Eleza kwa kifupi manufaa/faida mbili na changamoto mbili za sera ya Tanzania ya Uhusiano wa Kimataifa.
5. Eleza kwa kifupi hatua nne za kuzingatia wakati wa kufundisha dhana ya haki za binadamu ili kuwajengea wanafunzi uwezo wa kubaini haki hizo.
6. Eleza kwa ufupi stadi nne ambazo mwalimu anapaswa kuwajengea wanafunzi ili wawe raia wema.
7. Kwa kutumia hoja nne eleza uhusiano uliopo baina ya Azimio la Kazi na Muhtasari wa somo la Uraia.
8. Toa mambo manne katika hotuba yako kama mgeni rasmi kwa wazazi wa shule ya msingi Mtakuja kubaini na kutambua umuhimu wa kufanya mitihani.
9. Eleza kwa kifupi mbinu nne unazoweza kutumia mwalimu kutunza zana za kufundishia na kujifunzia.
10. Eleza kwa kifupi kwa kutumia hoja nne juu ya umuhimu wa kuandaa Azimio la Kazi.

SEHEMU B (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

11. Eleza tofauti za majukumu ya Mahakama ya Rufaa na Mahakama Kuu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
12. Thibitisha kwa kutoa hoja tano kuonesha umuhimu wa kuwa na wabunge kutoka vyama vya upinzani ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
13. Kwa kutumia hoja sita, chambua changamoto tano za kiuchumi zinazoweza kuikabili nchi inayoendelea kama Tanzania.
14. Kwa kutumia mifano mitano eleza namna wafanyabiashara wa Tanzania wanavyonufaika na uchumi wa soko huria.